JESUS
316

# Yesu ni nani?

**Yesu ni nani?** Biblia inatupa jibu pekee halisi kwa swali hilo. Mtume Paulo aliandika, *"Maandiko yote yamevuviwa na Mungu,"* 2 Timotheo 3:16. Biblia iliyovuviwa na Mungu, katika Mwanzo hadi Ufunuo, inafundisha kuwa Yesu ni Mungu tangu umilele uliopita hadi umilele ujao. Biblia inasema kuwa Yeye ndiye *"Alfa na Omega aliyeko, aliyekuwako na atakayekuja,"* Ufunuo 1:8. Biblia inamtambulisha Yesu kuwa Mungu, Muumba, Mchungaji Mkuu, Bwana, Mkombozi, Mwana-Kondoo wa Mungu, Bwana wa Mabwana, Mfalme wa Wafalme, Imanueli (Mungu pamoja nasi), Mwokozi, Kuhani Mkuu, na Ufufuo na Uzima.

**Yesu alikuwa Muumba.** *"Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Vitu vyote viliumbwa kupitia kwake, Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba,"* dondoo kutoka Yohana 1:1-14. *"Kwake yeye vitu vyote vilivyo mbinguni na juu ya nchi viliumbwa: vitu vinavyoonekana na visivyoonekana, viwe ni viti vya utawala au falme, au wenye mamlaka au watawala; vitu vyote viliumbwa kupitia kwake na kwa ajili yake.,"* dondoo kutoka Wakolosai 1:16-17.

**Yesu ndiye "MIMI NIKO".** Yesu, Malaika wa Bwana, alimwita Musa kutoka kwenye Kichaka Kilichokuwa Kinawaka Moto katika Kutoka 3 (~1,450 KK) na kujitambulisha kama *"MIMI NIKO"*. Katika Yohana 8, Yesu alijitangaza mwenyewe kuwa "MIMI NIKO" mkuu aliyekuwepo kabla ya Abrahamu (~2,100 KK) na kabla ya Wayahudi. Wayahudi waliona hilo kama dai lake la kuwa Mungu na wakaokota mawe ili kumuua. Baadaye, Yesu alisema *"Mimi na Baba yangu tu umoja,"* Yohana 10:30-31. Na Wayahudi wakainua mawe tena ili wampige nayo.

**Yesu yuko katika Agano la Kale.** Hakuna mtu yeyote aliyemwona Mungu Baba, Yohana 1:18, 6:46. Hata hivyo, Mungu akiwa Yesu aliyekuwako kabla ya kupata mwili alitokea watu kadhaa katika nyakati za Agano la Kale kabla hajazaliwa huko Bethlehemu. Alitokea kama Malaika wa Bwana kwa Hajiri katika Mwanzo 16 na 21, kwa Musa katika Kutoka 3, kwa Gideoni katika Waamuzi 6 na kwa wazazi wa Samsoni katika Waamuzi 13. Yesu alimtokea Abrahamu pia katika Mwanzo 18 & 22 na Yakobo katika Mwanzo 31 & 32. Na Yesu anatajwa kuwa mmoja katika Utatu katika Isaya 48:12-19 (kilichoandikwa yapata 700 KK).

**Yesu Ndiye aliyetabiriwa.** Zaidi ya unabii 300 wa Agano la Kale, kutoka mamia ya miaka mapema, unaelezea kuzaliwa, maisha na kifo cha Yesu. Baadhi ya unabii huo katika Zaburi 22 unatoa maelezo ya kutisha ya kusulubishwa kwake (kilichoandikwa yapata 1,000 KK wakati kupigwa kwa mawe kulikuwa ndio njia ya kumuua mtu). Utimizo wa unabii huo wa Zaburi ya 22 umeandikwa katika Mathayo 27.

**Yesu alifanyika Mungu-Mtu.** Nabii Isaya alitabiri kuwa *"kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto wa kiume,"* Isaya 9:6. Isaya alimtambulisha huyo kuwa ndiye Mungu mwenye nguvu. Mwana wa milele alitolewa kama mtoto aliyezaliwa huko Bethlehemu. Yesu alikuwepo kabla hajazaliwa - tangu umilele uliopita. Jina "Mwana wa Mungu" linaeleza cheo chake wala si kuzaliwa kwake. Haimaanishi kuwa alianza kuwepo wakati wa kuzaliwa kwake huko Bethlehemu. Mtume Paulo aliandika hivi, *"Kuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu: Yeye, ingawa alikuwa na asili ya Mungu hasa, hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa kitu cha kushikilia, bali alijifanya si kitu, akachukua hali hasa ya mtumwa, naye akazaliwa katika umbo la mwanadamu. Naye akiwa na umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza, akatii hata mauti: naam, mauti ya msalaba,"* Wafilipi 2:5-8. Yesu alifanyika binadamu kamili akiwa bado angali Mungu. Yesu wa milele, aliyekuwepo hapo awali alishuka kutoka Mbinguni na kuwa binadamu, Yohana 3:13, 31, Yohana 6:33-38. Yesu alikuwa Mungu na binadamu kwa wakati mmoja.

**Yesu alifanya miujiza.** Miujiza yake mingi inapatikana katika Agano Jipya. Miujiza tatu iliambatana na kujitambulisha kwake kwa njia ya ajabu. Alilisha watu 5,000 kimiujiza kisha akasema, *"Mimi ndimi mkate wa uzima,"* Yohana 6:35. Alimponya kipofu baada ya kusema, *"Wakati niko ulimwenguni, mimi ni nuru ya ulimwengu,"* Yohana 9:1-8. Yesu akamwambia, *"Mimi ndiye huo ufufuo na uzima. Yeye aniaminiye mimi, hata akifa atakuwa anaishi,"* Yohana 11:25. Kisha Yesu akaenda kwenye kaburi la rafiki yake Lazaro ambaye alikuwa amekufa kwa siku nne na kumfufua. Yesu aliwaponya wagonjwa, vilema, viziwi, bubu, wenye ukoma na watu waliopagawa. Aligeuza maji kuwa divai, akatembea juu ya maji na kutuliza bahari. Mathayo 9:2-7 inasimulia kuhusu wanaume waliomleta mtu aliyepooza kwa Yesu.

Akamwambia yule mtu *“mwanangu, jipe moyo mkuu. Dhambi zako zimesamehewa.”* Viongozi wa kidini walifikiri kuwa hiyo ilikuwa ni kukufuru kwa sababu ni Mungu pekee anayeweza kusamehe dhambi. Yesu akawauliza, *“Je, ni lipi lililo rahisi zaidi: kusema, ‘Umesamehewa dhambi zako,’ au kusema, ‘Inuka, uende’? Lakini nataka mpate kujua kwamba Mwana wa Adamu ana mamlaka duniani kusamehe dhambi.” Ndipo akamwambia yule aliyepooza, “Inuka, chukua mkeka wako, uende nyumbani mwako.’ Yule mtu akasimama, akaenda nyumbani mwake.”*

**Yesu alithibitisha kuwa alikuwa Mungu.** Yesu alitimiza unabii wa Agano la Kale kuhusu kuzaliwa, maisha na kifo chake. Alifanya miujiza mingi ili kuonyesha kuwa alikuwa Mungu. Alifundisha kwa mamlaka. *“Yesu alipomaliza kusema maneno haya, umati wa watu wakashangazwa sana na mafundisho yake, kwa sababu alifundisha kama yeye aliye na mamlaka, wala si kama walimu wao wa sheria,”* Mathayo 7:28-29. Naye aliishi maisha yasiyo na dhambi, Waebrania 4:15, 1 Petro 2:22, 1 Yohana 3:5. Yesu, kama Mungu-Mtu asiye na dhambi, alifanyika Mwanakondoo mkamilifu wa Mungu aliyetolewa dhabihu msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. *“Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, ili tufe kwa mambo ya dhambi, na tupate kuishi katika haki,”* 1 Petro 2:24.

**Yesu alisulubishwa na kufufuka kutoka kwa wafu.** *“Hamkukombolewa kwa vitu viharibikavyo kama fedha na dhahabu, bali mlikombolewa kwa damu ya thamani ya Kristo, yule Mwana-Kondoo asiye na dosari wala doa,”* 1 Petro 1:18-19. *“Wakamuua kwa kumtundika msalabani. Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu siku ya tatu na akamwezesha kuonekana na watu - Manabii wote walishuhudia juu yake kwamba kila mtu amwaminiye hupokea msamaha wa dhambi katika Jina lake,”* Matendo 10:39-40, 43. *“Kwa maana yale niliyopokea ndiyo niliyowapa ninyi, kama yenye umuhimu wa kwanza: Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama Maandiko yanavyosema, ya kuwa alizikwa na alifufuliwa siku ya tatu, kama Maandiko yanavyosema,”* 1 Wakorintho 15:3-4. Yesu alifufuka kutoka kaburini na alionekana na mashahidi wengi kabla ya kupaa kurudi Mbinguni.

**Yesu ndiye njia pekee ya kwenda kwa Mungu.** Yesu akawaambia, *“Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kupitia kwangu,”* Yohana 14:6. Mtume Petro alisema, *“Wala hakuna wokovu katika mwingine yeyote, kwa maana hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu linalopasa kutuokoa,” Matendo 4:12. Mtume Paulo aliandika, “Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani mwanadamu Kristo Yesu, aliyejitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wanadamu wote”* 1 Timotheo 2:5-6. Njia ya Yesu ya kwenda kwa Mungu ni tofauti na dini zingine zote. Hazitoi suluhisho kwa tatizo letu la dhambi. Zinafundisha kuwa ikiwa utafanya mema kwa ujumla kulingana na ufafanuzi wao tofauti wa mema na mabaya, basi miungu yao inaweza kupuuza dhambi yako na kukuruhusu uingie Mbinguni. Njia ya Yesu ni kuwa kwa kumwamini yeye dhambi zako zinalipwa msalabani na unasamehewa. Ukiwa na Yesu unaenda Mbinguni ukiwa umesamehewa. *“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele,”* Yohana 3:16.

**Yesu atarudi tena**. Yesu alisema, *“Msifadhaike mioyoni mwenu. Mnamwamini Mungu, mniamini pia. Nyumbani mwa Baba yangu kuna makao mengi. Kama sivyo, ningewaambia. Naenda kuwaandalia makao. Nami nikienda na kuwaandalia makao, nitarudi tena na kuwachukua mkae pamoja nami, ili mahali nilipo nanyi mpate kuwepo.”* Yohana 14:2-3. Na katika maneno ya mwisho ya Biblia, Yesu alisema “Hakika, naja upesi.” Mtume Yohana aliongeza, “Amen. Njoo, Bwana Yesu,” Ufunuo 22:20-21. Ikiwa Yesu angerudi leo, ungekuwa tayari kukutana naye? Tembelea www.Gospel316.org ili kuhakikisha kuwa uko tayari kwa kumwamini Yesu na kusamehewa na Mungu.

**Yesu ni Mungu tangu umilele uliopita hadi umilele ujao.**

**Pata mshangao wa kustaajabisha kwa kutajwa kwa jina lake!**

*Yesu ni nani?* © 2025 iliyoandikwa na John D. Morris III ilichapishwa na Acts One Eight. Unaweza kuchapisha, kunakili, kuchapisha mtandaoni, kutuma kwa barua pepe au kutuma kwa ujumbe wa simu bila malipo bila kubadilisha maudhui yake ikiwa na taarifa hii kamili. Unaweza kuongeza jina au nembo ya huduma au kanisa lako kwenye sehemu ya juu ya ukurasa wa kwanza na uongeze maelezo yako ya mawasiliano juu ya mstari ulio karibu na sehemu ya chini ya ukurasa wa pili. Maudhui ya Jesus316 yana msingi wake kwenye Biblia pekee. Ipo ili kuwasaidia watu kuweka imani katika Yesu Kristo na kisha kukua na kuwa wanafunzi wake. Unaweza kutuma barua pepe kwa Acts One Eight (kwa Kiingereza ikiwezekana) kwa: Hello@Mail316.org. Huduma za tafsiri kwa matoleo yasiyo ya Kiingereza zilitolewa na www.ChristianLingua.com. *Yesu ni nani?* inapatikana katika lugha 48 bila malipo kwenye www.Jesus316.org. Nukuu za Biblia katika toleo la Kiingereza zilitoka katika New American Standard Bible ya The Lockman Foundation ya 1995. Nukuu za Biblia katika tafsiri hii zinatoka kwenye Kiswahili Contemporary Version (NENO) Hakimiliki © 1984, 1989, 2009,2015 ya Biblica Inc.